
TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

# MWELEKEO WA MVUA ZA MSIMU WA MASIKA
# MACHI – MEI, 2026




***Kielelezo 1: Mwelekeo wa mvua za Machi hadi Mei, 2026.***


*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz


**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

## Dondoo muhimu za msimu wa mvua za Masika (Machi – Mei), 2026

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mwelekeo wa mvua za Masika kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka (kanda ya Ziwa Victoria, nyanda za juu kaskazini mashariki, pwani ya kaskazini pamoja na maeneo yaliyopo kaskazini mwa mkoa wa Kigoma) katika kipindi cha miezi ya Machi hadi Mei, 2026. Ushauri na tahadhari umetolewa kwa wadau wa sekta mbalimbali wanaotumia taarifa za hali ya hewa katika utekelezaji wa majukumu yao kama vile kilimo na usalama wa chakula, mifugo na uvuvi, maliasili, wanyamapori na utalii, nishati na madini, maji, ujenzi, usafiri na usafirishaji (nchi kavu, kwenye maji na angani), mamlaka za miji, afya, sekta binafsi pamoja na menejimenti za maafa. Muhtasari wa mwelekeo wa mvua hizo na athari zake ni kama ifuatavyo:

**a) Mwelekeo wa mvua za Masika kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka:**

i. Mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya pwani ya kaskazini pamoja na baadhi ya maeneo ya magharibi mwa ukanda wa Ziwa Viktoria (mikoa ya Kagera na Geita) pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma. Aidha, mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zinatarajiwa katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki na baadhi ya maeneo ya ukanda wa Ziwa Viktoria (mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara na Simiyu).

ii. Mvua za Masika zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Februari na ya kwanza ya mwezi Machi , 2026 katika maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria; na wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Machi katika maeneo ya pwani ya kaskazini; na wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Machi, 2026 katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki. Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya nne ya mwezi Mei na wiki ya kwanza ya mwezi Juni 2026 katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka.

iii. Ongezeko la mvua linatarajiwa mwezi Aprili, 2026.

**b) Athari zinazotarajiwa:**

i. Vipindi vya unyevu wa kuzidi kiasi pamoja na mafuriko vinaweza kujitokeza na kuathiri ukuaji wa mazao katika baadhi ya maeneo, hususan yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani.

ii. Kina cha maji katika mito, mabwawa na hifadhi ya maji ardhini kinatarajiwa kupungua hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani.

iii. Magonjwa ya mlipuko yanaweza kujitokeza kutokana na uchafuzi wa maji.

1. **MWENENDO WA MVUA ZA MSIMU (NOVEMBA, 2025 HADI APRILI, 2026) NA MWELEKEO WA MVUA ZA MASIKA (MACHI – MEI), 2026**

## *1.1 Mwenendo wa mvua za Msimu (Novemba, 2025 hadi Aprili, 2026)*

Mvua za Msimu ambazo utabiri wake ulitolewa mwezi Oktoba, 2025 zilitarajiwa kuwa za Chini ya Wastani hadi Wastani katika maeneo ya mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Singida na Dodoma. Aidha, mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zilitarajiwa katika mikoa Njombe, Iringa, Mbeya, Songwe, Rukwa, Ruvuma, Mtwara, Lindi, pamoja na kusini mwa mkoa wa Morogoro.

Mvua hizi zilianza mapema wiki ya nne ya Oktoba na wiki ya kwanza ya Novemba, 2025 katika maeneo mengi ya Magharibi mwa nchi na kufuatiwa na maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi wiki ya pili ya mwezi Novemba kama ilivyotabiriwa. Aidha, ongezeko la mvua lilijitokeza zaidi mwezi Desemba, 2025 katika maeneo mengi. Katika kipindi kilichosalia cha msimu (Februari hadi Aprili, 2026) mvua zinatarajiwa kuendelea kama ilivyotabiriwa.

## *1.2 Mwelekeo wa mvua za Masika (Machi hadi Mei), 2026*

Msimu wa mvua za Masika ni mahususi kwa maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), pwani ya kaskazini (kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, mkoa wa Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia), Dar es Salaam, Tanga pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), ukanda wa Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu na Mara) pamoja na kaskazini mwa Mkoa wa Kigoma.

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa inayotarajiwa katika kipindi cha Masika (kama inavyoelezwa katika kipengele Na. 2 cha taarifa hii), mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya pwani ya kaskazini pamoja na baadhi ya maeneo ya magharibi mwa ukanda wa Ziwa Viktoria (Hususan mikoa ya Kagera, Geita na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma). Aidha, mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya nyanda za juu kaskazini mashariki pamoja na baadhi ya maeneo ya ukanda wa Ziwa Viktoria (mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara na Simiyu). Ongezeko la mvua linatarajiwa mwezi Aprili, 2026. Maelezo ya kina juu ya mwelekeo wa mvua za msimu ni kama ifuatavyo:

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

i. **Kanda ya Ziwa Victoria: (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu na Mara) pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma (wilaya za Kakonko na Kibondo):**


Mvua za Masika zinatarajiwa kuwa za Wastani hadi Juu ya Wastani katika baadhi ya maeneo ya magharibi mwa ukanda wa Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita) pamoja na kaskazini mwa Mkoa wa Kigoma. Aidha, mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zinatarajiwa katika maeneo ya mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara na Simiyu. Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Februari na wiki ya kwanza ya mwezi Machi na kuisha wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Mei, 2026.

ii. **Ukanda wa Pwani ya Kaskazini: (kaskazini mwa Mkoa wa Morogoro, Pwani (ikijumuisha kisiwa cha Mafia), Dar es Salaam, Tanga pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):**

Mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya ukanda wa pwani ya kaskazini. Mvua hizo zinatarajiwa kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Machi na kuisha wiki ya nne ya mwezi Mei na wiki ya kwanza ya mwezi Juni, 2026.

iii. **Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki: (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):**

Mvua katika maeneo haya zinatarajiwa kuwa za Wastani hadi Chini ya Wastani na zinatarajiwa kuanza wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Machi na kuisha wiki ya nne ya mwezi Mei, 2026.




*Kielelezo 2: Kushoto: Mwelekeo wa mvua za Masika (Machi –Mei), 2026 na Kulia: Wastani wa muda mrefu (miaka 30) wa mvua za Masika (1991-2020).*

***Angalizo 1:*** *Izingatiwe kuwa matukio ya hali mbaya ya hewa ikiwemo vipindi vya mvua kubwa yanaweza kujitokeza hata katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani.*

***Angalizo 2:*** *Mwelekeo wa mvua uliotolewa umezingatia zaidi kipindi cha mvua za Masika (miezi mitatu) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya mvua na mabadiliko ya muda mfupi vitazingatiwa katika utabiri wa kila siku na utabiri wa kila mwezi. Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia taarifa za utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi na tahadhari kama zinavyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).*

## 2. MIFUMO YA HALI YA HEWA

Joto la bahari katika eneo la mashariki mwa Bahari ya Hindi (Pwani ya Indonesia) linatarajiwa kuwa juu kidogo ya wastani, wakati eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi (pwani ya Afrika Mashariki) likitarajiwa kuwa na joto la Bahari la wastani. Hali hii inatarajiwa kupunguza kwa kiasi kidogo upepo wenye unyevunyevu kuvuma kuelekea katika maeneo ya pwani ya nchi yetu na maeneo jirani.

Aidha, Joto la bahari katika eneo la Tropiki ya kati ya Bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuwa la Wastani hadi Juu kidogo ya Wastani. Hali hii inatarajiwa kuwa na mchango hafifu katika kuimarisha mifumo isababishayo mvua hapa nchini.

Kwa upande mwingine, mabadiliko madogo ya upepo wa magharibi yanatarajiwa katika maeneo ya mashariki mwa Congo hususan katika kipindi cha kuelekea mwishoni mwa msimu. Hali hii inatarajiwa kuimarisha kwa kiasi kidogo upepo wenye unyevunyevu kuvuma kuelekea katika maeneo ya magharibi mwa ukanda wa Ziwa Victoria na hivyo kuimarisha kwa kiasi kidogo mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

## 3. ATHARI NA USHAURI

Athari za kisekta na ushauri uliotolewa hapa chini umeandaliwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kwa kushirikiana na wataalam wa sekta husika katika mkutano wa wadau wa hali ya hewa uliofanyika tarehe 2 Februari, 2026, na pia mkutano na Wanahabari uliofanyika tarehe 4 Februari, 2026. Wadau wa sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii wanashauriwa kupanga na kutekeleza shughuli zao kwa kuzingatia taarifa mahususi za hali ya hewa zinazotolewa na TMA.

### a) Kilimo na Usalama wa Chakula

Vipindi vya unyevu wa kuzidi kiasi pamoja na mafuriko vinaweza kujitokeza na kuathiri ukuaji wa mazao katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani. Hali hii inaweza kuathiri ukuaji wa mazao kutokana na wingi wa maji unaoambatana na upotevu wa virutubisho muhimu kwenye udongo. Vilevile, wadudu

waharibifu kama vile panya na mchwa na magonjwa ya mimea yanayoendana na hali ya ongezeko la unyevu kama vile ukungu yanatarajiwa kuongezeka na kuathiri mazao kama ndizi, mahindi, maharage, mihogo na mpunga. Maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani yanaweza kukumbwa na upungufu wa unyevu, ambao unaweza kuathiri ukuaji wa mimea na kusababisha upungufu wa mavuno hususan kwa mazao yanayotegemea mvua.

Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba kwa wakati, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa kuzingatia hali ya unyevu katika udongo. Aidha, wanashauriwa kutumia mbinu bora na teknolojia za kuzuia maji kutuama shambani, kuzuia mmomonyoko wa udongo na upotevu wa rutuba kutokana na kutuwamisha maji kwa muda mrefu au mafuriko, na kuhifadhi maji shambani kwenye maeneo yanayotarajia kupata upungufu wa mvua. Vilevile, inashauriwa kuimarisha miundombinu ya kilimo na kudhibiti kwa wakati visumbufu na magonjwa ya mimea ili kupunguza madhara yanayoweza kujitokeza. Aidha, wakulima wanashauriwa kutumia mbinu za uvunaji wa maji ya mvua ili yaweze kutumika kwa umwagiliaji kipindi cha ukavu.

Wakulima wanashauriwa kutafuta taarifa sahihi kutoka kwa maafisa ugani kwa kuzingatia utabiri wa msimu wa wilaya husika katika kuandaa na kuchagua zao, mbegu na pembejeo sahihi. Aidha, wakulima, maafisa ugani na wadau wengine wa kilimo kama vile watafiti wanashauriwa kuendelea kufuatilia na kutumia utabiri wa siku na wa siku kumi ili kuwawezesha kutekeleza shughuli za kilimo kwa usahihi.

**b) Mifugo na Uvuvi**

Katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani upungufu wa maji unaweza kujitokeza na hivyo unaweza kuathiri upatikanaji wa maji na malisho ya mifugo na kusababisha migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Vilevile, katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani, wafugaji na wavuvi wanatarajiwa kunufaika na upatikanaji wa malisho, maji na chakula cha samaki. Aidha, kilimo cha mwani kinaweza kuathirika kutokana na upungufu wa chumvi chumvi baharini. Hata hivyo, milipuko ya magonjwa ya mifugo kama vile homa ya bonde la ufa, kuongezeka kwa magonjwa yaenezwayo na kupe, changamoto ya kuongezeka kwa minyoo na kuzaliana kwa wadudu/wanyama wadhurifu kunaweza kujitokeza.

Wafugaji wanashauriwa kuweka mipango mizuri ya matumizi na uhifadhi wa maji na vyakula vya mifugo. Aidha, Wafugaji na Wavuvi wanashauriwa kutumia taarifa za utabiri wa hali ya hewa na kuzingatia ushauri unaotolewa na maafisa Ugani ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza na kuendelea kunufaika na hali ya hewa inayotarajiwa wakati wa msimu.

### c) Utalii na Wanyamapori

Mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zinazotarajiwa zinaweza kusababisha uhaba wa malisho na maji kwa wanyamapori katika mbuga na mapori ya akiba na hivyo kusababisha migogoro kati ya wanyamapori na jamii inayowazunguka. Hata hivyo, mvua nyingi zinaweza kusababisha kutuama na kusambaa kwa maji na kusababisha kuhama kwa wanyamapori, hasa katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani. Hali hii inaweza kusababisha maambukizi ya magonjwa kutoka kwa wanyamapori kwenda kwa wanyama wanaofugwa kutokana na wanyamapori kuingia katika maeneo ya jamii yanayozunguka hifadhi na mapori ya akiba. Pia, hali hii inaweza kusababisha hatari kwa binadamu na wanyama wanaofugwa kutokana na kushambuliwa na wanyama pori.

Mamlaka husika zinashauriwa kuboresha miundombinu mbalimbali katika mbuga na mapori ya akiba na kujenga uelewa kwa jamii ili kuchukua hatua stahiki kutokana na athari zinazoweza kujitokeza. Hivyo, jamii inashauriwa kutoa taarifa kwa mamlaka husika pindi wanyamapori wanapoingia katika maeneo yao ya makazi.

### d) Ujenzi

Sekta ya Ujenzi inatarajiwa kunufaika hususani katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani katika msimu huu wa Masika. Kwa upande mwingine, katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani shughuli za ujenzi, hususan mpangilio wa kazi unaweza kuathiriwa, gharama za ujenzi zinaweza kuongezeka na hivyo kupelekea kuchelewa kwa ukamilishaji wa baadhi ya miradi. Wadau wa sekta ya ujenzi wanashauriwa kuzingatia taarifa ya utabiri huu na utabiri wa kila siku katika mpangilio wa kazi na utekelezaji wa miradi ya ujenzi.

### e) Usafiri na Usafirishaji

Kwa ujumla, Sekta ya Usafiri na Usafirishaji inatarajiwa kunufaika kutokana na mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani katika msimu huu wa Masika. Kwa upande mwingine, maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani; matukio ya uharibifu wa miundombinu ya barabara na reli sambamba na kuongezeka kwa ajali za usafiri wa nchi kavu yanaweza kujitokeza. Aidha, matukio ya kuchelewa, kuahirishwa kwa safari za ndege na kwenye maji pamoja na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji katika Sekta ya Usafiri wa Anga na kwenye maji yanaweza kujitokeza. Wadau wa sekta hii wanashauriwa kuchukua hatua stahiki ikiwemo kufuatilia na kuzingatia utabiri wa kila siku, na tahadhari za kiusalama na ukaguzi wa mara kwa mara wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji ili kupunguza madhara yanayoweza kujitokeza.

### f) Nishati, Maji na Madini

Kupungua kwa kina cha maji katika mito, mabwawa na hifadhi ya maji ardhini kunatarajiwa kujitokeza hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Chini ya

Wastani. Ongezeko la vina vya maji katika mabwawa na mito linatarajiwa kujitokeza hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani na hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa matukio ya mafuriko hususan katika maeneo yanayoathiriwa zaidi na mafuriko.

Upungufu wa maji unaweza kupelekea ongezeko la gharama za kutibu maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Aidha mafuriko yatapelekea kuongezeka kwa gharama za kutibu maji kutokana na uchafuzi wa vyanzo vya maji. Matumizi endelevu ya rasilimali maji yanasisitizwa hususan katika shughuli za umwagiliaji, uzalishaji wa umeme wa maji, shughuli za uchenjuaji wa madini, matumizi ya viwandani na nyumbani. Aidha, jamii na Mamlaka za Nishati na Maji zinashauriwa kuchukua hatua stahiki ili kuepuka athari zinazoweza kuathiri miundombinu ya maji na nishati.

**g) Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zinazotarajiwa katika maeneo mengi zinaweza kupelekea upungufu wa upatikanaji wa maji kwa matumizi ya nyumbani, kilimo na ufugaji. Hivyo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuchukua hatua madhubuti ikiwemo kuimarisha na kuboresha mifumo ya usambazaji maji safi ili kuhakikisha upatikanaji wa kutosha wa maji katika kaya na sekta nyingine. Aidha, vipindi vya mvua kubwa katika baadhi ya maeneo vinaweza kusababisha kutuama kwa maji na mafuriko. Hali hii inaweza kusababisha uharibifu wa miundombinu na upotevu wa maisha na mali. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuboresha mifumo ya mifereji ya maji ili kupunguza athari zinazoweza kusababishwa na mafuriko sambamba na kutoa elimu kwa jamii juu ya hatua zinazopaswa kuchukuliwa katika utekelezaji wa shughuli za kijamii na kiuchumi

Vilevile, Mamlaka husika zinashauriwa kuongeza uelewa kwa Timu za Usimamizi wa Halmashauri kupitia vikao vyake halali, Baraza la Madiwani na Vikao vya Kamati ya Ushauri ya Wilaya, kuhusu hali ya msimu unaotarajiwa na kuhamasisha uandaaji wa mipango na bajeti mahsusi kwa kila sekta ili kuongeza utayari na kupunguza athari zinazoweza kujitokeza. Aidha, tunashauri Mamlaka za Miji na Serikali za Mitaa kuwa na Mpango wa muda mrefu wa kuwawezesha wananchi kuhimili mabadiiiko ya tabianchi/hali ya hewa. Hii ni pamoja na kuimarisha Kamati za Maafa kuanzia ngazi ya kijiji hadi wilaya ili kusimamia na kupunguza athari hizo.

**h) Sekta ya Afya**

Maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani, jamii inaweza kulazimika kutumia maji yasiyo safi na salama hivyo hatua stahiki za kiafya zinashauriwa kuzingatiwa ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza. Maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Juu ya wastani, uharibifu wa miundombinu ya maji unaoweza kusababishwa na maji ya mvua kutuama na kutiririka katika makazi ya watu unaweza kusababisha uchafuzi wa maji na hivyo kusababisha kutokea kwa magonjwa ya mlipuko yanayohusiana na maji machafu na wadudu wadhurifu.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

Mamlaka za Afya na jamii zinashauriwa kuchukua hatua stahiki kwa kuzingatia makundi maalum ili kupunguza athari hasi za kiafya zinazotarajiwa kwa kuharibu mazalia ya mbu, kutibu maji kabla ya kuyatumia, kunywa maji safi na salama pamoja na kuhakikisha uwepo wa dawa na vifaa tiba vya kutosha katika vituo vya Afya.

### i) Sekta Binafsi

Shughuli za kilimobiashara na uzalishaji viwandani zinaweza kuathirika kutokana na upungufu wa malighafi za kilimo utakaotokana na upungufu wa mvua hususan kwenye maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani. Hali hii, inaweza kusababisha ongezeko la gharama za upatikanaji wa malighafi na uendeshaji. Aidha, upungufu wa mvua unaweza kuathiri ubora wa bidhaa mfano miti ya nguzo, mbao, nyama na asali.

Wadau wa Sekta Binafsi wanashauriwa kushirikiana na wataalamu mbalimbali ikiwemo wataalam wa hali ya hewa ili kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza. Taasisi za Benki, Taasisi za Mikopo na Bima zinashauriwa kuandaa na kutoa huduma mahususi kwa wadau ili kuwajengea ustahimilivu katika biashara.

### j) Menejimenti za Maafa

Hali ya upungufu wa mvua inatarajiwa katika baadhi ya maeneo, hususan yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani. Hali hii inaweza kusababisha upungufu wa maji safi na salama, kupungua kwa uzalishaji wa chakula, na uhaba wa malisho kwa mifugo. Vilevile, vipindi vifupi vya mvua kubwa vinaweza kujitokeza na kusababisha mafuriko na maporomoko ya ardhi. Matukio haya yanaweza kuleta uharibifu wa miundombinu na mazingira, milipuko ya magonjwa, pamoja na upotevu wa mali na maisha. Idara ya Usimamizi wa Maafa, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali nchini, inashauriwa kuendelea kuratibu na kutekeleza mipango ya kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

Aidha, Sekta ya Mazingira pamoja na Kamati za Usimamizi wa Maafa katika ngazi za mikoa, wilaya, kata/shehia, na kijiji/mtaa zinashauriwa kuchukua hatua stahiki, ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kuhusu maafa kwa kuzingatia sera, sheria, taratibu na miongozo itakayosaidia katika kuzuia/kupunguza athari, kujiandaa, kukabiliana na kurejesha hali pindi maafa yatakapotokea pamoja na kuhamasisha uhifadhi wa chakula kwa jamii.

### k) Vyombo vya Habari

Waandishi wa habari wanashauriwa kufuatilia na kusambaza kwa wakati taarifa sahihi za utabiri na tahadhari za hali ya hewa kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kwa lengo la kuhabarisha jamii na kusaidia kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza. Ikumbukwe kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Na. 2 ya Mwaka 2019, ni kosa kisheria kusambaza taarifa kutoka katika vyanzo visivyo rasmi.

Pia, wanashauriwa kushirikiana na wataalamu wa sekta mbalimbali ili kuandaa na kusambaza Makala na Ripoti mbalimbali za hali ya hewa zenye lugha rahisi, zitakazosaidia

jamii kutumia taarifa hizo katika kupanga na kukabiliana na athari za hali ya hewa zinazoweza kujitokeza.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kuzingatia ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa mirejesho ya mwelekeo wa mvua nchini kadri inavyohitajika. Aidha, wadau wanashauriwa kuwasiliana na Mamlaka ili kupata taarifa mahsusi za utabiri wa msimu ili kukidhi mahitaji maalum katika sekta zao.*

***Imetolewa: Tarehe 5 Februari , 2026.***
**Na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania:**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz